TANGAZO LA SERIKALI NA. 7 la tarehe 4/1/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA. NA. 272)

# AMRI

*(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu Na.28 (d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MUSOMA ("MUSOMA WSSA") (YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2019

Kichwa cha Amri

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma ("Musoma WSSA")(ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2019.

Tarehe ya kuanza

2. Amri hii itaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Januari 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Musoma WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo-

(a) ifikapo tarehe 30 Aprili 2019 au kabla, Musoma WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(b) ifikapo tarehe 30 Aprili 2019 au kabla, Musoma WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa namna ya kuthibiti maji yanayopotea;

(c) Musoma WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii;

(d) Musoma WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii;

(e) Musoma WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa;

(f) Musoma WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Musoma WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Musoma WSSA katika siku zijazo.

Kutenguliwa kwa Amri

5. Amri hii inatengua matumizi ya Amri Na. 13-004 ya tarehe 28 Juni 2013 katika maeneo yanayohudumiwa na Musoma WSSA.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

Bei, Ada na Tozo Zilizoidhinishwa

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

| Kundi la wateja | Matumizi | Bei ya sasa | Bei iliyoopendekezwa | | | Bei iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 0-5m$^3$ | 850 | 2,310 | 2,422 | 2,574 | 990 | 1,040 | 1,040 |
| | 5-10m$^3$ | 990 | 2,691 | 2,821 | 2,998 | 1,150 | 1,210 | 1,210 |
| | Above 10m$^3$ | 1,090 | 2,963 | 3,106 | 3,301 | 1,260 | 1,330 | 1,330 |
| Taasisi | 0-30m$^3$ | 1,140 | 3,099 | 3,248 | 3,452 | 1,320 | 1,390 | 1,390 |
| | Above 30m3 | 1,250 | 3,398 | 3,562 | 3,785 | 1,450 | 1,520 | 1,520 |
| Biashara | 0-30m$^3$ | 1,230 | 3,343 | 3,505 | 3,725 | 1,430 | 1,500 | 1,500 |
| | Above 30m$^3$ | 1,340 | 3,642 | 3,818 | 4,058 | 1,550 | 1,630 | 1,630 |
| Viwanda | 0-50m$^3$ | 1,260 | 3,425 | 3,590 | 3,815 | 1,460 | 1,530 | 1,530 |
| | Above 50m$^3$ | 1,340 | 3,642 | 3,818 | 4,058 | 1,550 | 1,630 | 1,630 |
| Magati | | 550 | 1,495 | 1,567 | 1,665 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |

Schedule 1 (b): Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

| Kundi la wateja | Bei ya sasa | Bei iliyopendekezwa | | | Bei iliyoishinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 20% ya gharama ya maunganisho kama ilivyo tajwa kwenye sehemu ya 24 ya kanuni ya mwaka 2013 | 500,000 | 520,000 | 540,800 | 20% ya gharama ya maunganisho kama ilivyo tajwa kwenye sehemu ya 24 ya kanuni ya mwaka 2013 | | |
| Biashara | | 200,000 | 208,000 | 500,000 | | | |
| Taasisi | | 500,000 | 520,000 | 500,000 | | | |
| Viwanda | | 100,000 | 104,000 | 1,000,000 | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Magati | | 50,000 | 52,000 | - | |

Schedule 1 (c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

| Customer Category | Bei za Sasa | Bei Zilizopendekezwa | | | Bei zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 7,500 | 7,500 | 7,500 | 7,500 | 7,500 | 7,500 | 7,500 |
| Biashara | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 7,500 | 7,500 | 7,500 | 7,500 | 7,500 | 7,500 | 7,500 |

Schedule 1 (d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa kwa huduma ya Majitaka

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Bei Zilizopendekezwa | | | Bei zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | NA | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| Taasisi | NA | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| Biashara | NA | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Viwanda | NA | 100,000 | 100,000 | 100,000 | 100,000 | 100,000 | 100,000 |

JEDWALI LA PILI

Miradi Itakayotokelezwa

| Maelezo ya Kazi zitakazofanyika | Shilingi | | | Tarehe ya Mwisho ya Utekelezaji |
|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | |
| Ukarabati na Matengenezo | | | | |
| Kubadilisha valvu 30 chakavu na mbovu za milimeta 225 ifikapo Juni 2021 | 236 | 260 | 273 | Juni 2021 |
| Kubadilisha bomba chakavu kwa umbali wa kilimita 2km ifikapo Juni 2021 | 35 | 35 | 35 | Juni 2021 |
| Jumla Ndogo ya Mabadilisho | 271 | 296 | 308 | |
| Miradi Mipya | | | | |
| Uendelezaji wa bomba lenye kipenyo cha milimeta 150 kutoka Songe mpaka Bweri kwa umpbali wa km 1.2 ifikapo Juni 2020 | 15 | 10 | | Juni 2020 |
| Ununuzi na ufungaji wa meta kwa wateja wote wasio na meta ifikapo Juni 2021 | 259 | 585 | 765 | Juni 2021 |
| Ununuzi na ufungaji wa *generator* kwa ajili ya kusaidia uwekaji dawa pindi umeme unapokatika Juni 2019 | 75 | 75 | | Juni 2019 |
| Jumla ndogo ya uwekezaji mpya | 364 | 680 | 765 | |
| Jumla kuu ya gharama za uwekezaji | 635 | 976 | 1073 | |

JEDWALI LA TATU

Viashiria vya Utendaji (2018/19 – 2020/21)

| Maelezo | Uniti | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Idadi ya wateja wapya wa maji safi | Na | 2,000 | 2,000 | 3,000 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | % | 50% | 49% | 45% |
| Wateja wenye Dira | % | 80 | 90 | 100 |
| Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato | % | 90 | 92 | 95 |

Dodoma,
..............., 2018

NZINYANGWA E. MCHANY,
*Mkurugenzi Mkuu*